# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA RAIS
## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**Namba za Simu** Shule ya Sekondari Itilima

Mkuu wa Shule 0758189471 / 0682975853 S.L.P 184,

Makamu Mkuu wa Shule 0784317906 **BARIADI**

Matron 0786930980 29 / 03/ 2023

Mzazi/ Mlezi wa ___________________________________
S.L.P ______________________________

YAH: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ITILIMA HALMASHAURI YA WILAYA YA ITILIMA, MKOA WA SIMIYU MWAKA 2023**

1. Ninafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka 2023 tahasusi ya____________. Shule ya Sekondari Itilima iko Luguru, umbali wa kilometa 13 kusini mwa mji wa Bariadi. Usafiri wa basi kutoka mjini Bariadi unapatikana katika kituo cha mabasi mjini, nauli ni shilingi elfu mbili tu. (2,000/=)

   Muhula wa masomo utaanza tarehe 14/**08/2023** Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 13/**08/2023** Mwisho wa kuripoti ni tarehe 31/**08/2023.**

   Aidha kutakuwa na kikao cha wazazi wote wiki ya kwanza ya mwezi wa kumi, siku na tarehe ya kikao wazazi wote watafahamishwa kupitia simu za mkononi.

2. Mambo muhimu ya kuzingatia.

   2.1.Sare ya Shule.

   a) Sare ya Shule hii ni sketi mbili (2) za rangi ya Orange (kama rangi ya mtungi was gas wa ORYX), kitambaa cha suti kumbuka iwe ni sketi ndefu, inayofika kwenye vifundo vya miguu, itakayofunika kabisa miguu. sketi fupi hatoruhusiwa kabisa kuivaa. Maelekezo ya mshono na picha yameambatanishwa baada ya maelekezo.
   b) Shati mbili (2) nyeupe za tetron mikono mirefu.
   c) Koti jeupe la Maabara, Kwa mwanafunzi anayechukua Tahasusi za masomo ya Sayansi.
   d) Rangi ya hijab (kijuba) ifanane na sare za shule (nyeupe) na baibui nyeusi kwa ajili ya kuendea msikitini.
   e) Sare ya michezo kwa shule hii ni track suti nyeusi moja (1), tisheti na suruali nyeusi jozi moja(1) (Jezi)
   f) Viatu vyeusi vya kufunga na kamba nyenye visigino vifupi jozi mbili (2).

g) Soksi jozi mbili (2) nyeupe (stocking)
h) Sweta nyeusi moja (1) isiwe na mapambo.
i) Nguo za kushindia (Shamba dress) rangi ya **BLUU BAHARI** (kama rangi ya mtungi wa gas wa Lake)kitambaa cha suti. Gauni mbili za bluu bahari zenye kola nyeupe.
j) Skafu (1) yenye utepe mweupe rangi ya kitambaa cha sketi
k) Raba nyeupe kwa ajili ya michezo



**MICHANGO YA SHULE.**

a) Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni:-

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Fedha zote za michango ziwekwe kwenye akaunti Na **30502300492 NMB**, yenye jina

**"ELIMU YA KUJITEGEMEA ITILIMA SEKONDARI"**

c) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-

i) Ream mbili (2) ya karatasi A4 kwa mwaka.

ii) Vitabu vya masomo ya tahasusi yake pamoja na madaftari makubwa (Counter books) Quire 4 saba.

iii) Dissecting Kit kwa wanafunzi wa Baiolojia.

iv) Four figure moja (I) kwa wanafunzi wa Jiografia na Hesabu.

v) Scientific calculator moja kwa wanafunzi wa Jiografia, Fizikia, Hesabu na Kemia.

vi) Mathematical set moja (l) kwa wanafunzi wa Jiografia na Hesabu.

vii) Godoro Ia futi $2\frac{1}{2}$ x 6

viii) Shuka mbili rangi ya Pinki, Chandarua I, blanketi I, Mto wa kulalia mmoja na foronya rangi ya Pinki.

ix) Vyombo vya chakula (Sahani, bakuli, kijiko na kikombe).

x) Ndoo mbili zenye mifuniko.

xi) Kwanja 1, Jembe 1, Reki I, Mfagio wa ndani I (soft bloom) na wa nje l (chelewa) kwa kila mwanafunzi.

xii) Galoni I Iita 5, kwa ajili ya maji ya kunywa.

NB: Mwanafunzi akumbuke kuja na mahitaji yake binafsi.

**3. MAKOSA YATAKAYOSABABISHAMWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;

vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. SHERIA ZA SHULE**

**4.1.HESHIMA NA MWENENDO**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku ( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**NB:** ***NI MARUFUKU KWA MWANAFUNZI KUMILIKI, KUTUMIA AU KUKUTWA NA SIMU YA MKONONI KATIKA MAZINGIRA YA SHULE. IKIBAINIKA, MBALI NA ADHABU NYINGINE, MWANAFUNZI ATATAKIWA KULIPA KIASI CHA SHILINGI 200,000/= KWA AJILI YA FIDIA UHARIBIFU WA MIUNDOMBINU YA UMEME.***

## 3. SHERIA ZA SHULE

### HESHIMA NA MWENENDO

i) Mwanafunzi anatakiwa kuwa na adabu njema, utii na nidhamu ya hali ya juu awapo shuleni na nje ya shule.

ii) Mwanafunzi akiwa nje ya darasa lazima asimame na kumsalimia mwalimu, mfanyakazi au mtu yeyote mkubwa kwa heshima na adabu.

iii) Mwanafunzi anatakiwa kusimama na kumsalimia mwalimu au mtu yeyote anapoingia darasani, maktaba na katika ukumbi wa mikutano.

iv) Mwanafunzi anapoitwa na mwalimu, mfanyakazi au mtu yeyote mkubwa yambidi atii wito na kukimbia mara moja maagizo halali anayopewa.

v) Mwanafunzi anatakiwa kuhesabu na kutunza mali ya Umma na ya mwanafunzi mwenzake.

vi) Mwanafunzi haruhusiwi kuiba popote, akipatikana na kosa la wizi ikithibitika anafukuzwa Shule. ( Summary Dismissal)

vii) a) Ni marufuku kwa mwanafunzi wa kike na kiume kuhusiana kimapenzi. Watakaobainika wanakiuka sheria hii, ikithibitishwa watafukuzwa shule wote wawili.

b) Mwanafunzi wa kike akibainika kuwa ni mjamzito au ametoa mimba atafukuzwa shule mara moja.

viii) Ni marufuku kunywa pombe, kutumia madawa ya kulevya au kuvuta bangi, ikibainika atafukuzwa shule mara moja.

ix) Ni marufuku kwa mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi katika eneo la shule. Akibainika hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake ikiwa ni pamoja na kunyang'anywa simu hiyo na kutorudishiwa kamwe.

x) Ni marufuku kuonekana kwenye maeneo ya nyumba za kulala wageni au klabu ya pombe.

### KUHUDHURIA MADARASANI NA KATIKA SHUGHULI ZA SHULE

i) Kusoma kwa bidii na kushughulikia mapungufu yako.

ii) Kila mwanafunzi anapaswa kuwahi darasani kila asubuhi.

iii) Mwanafunzi haruhusiwi kupiga kelele awapo darasani, haruhusiwi kutoka nje ya darasa bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi wa darasa lake.

iv) Mwanafunzi anatakiwa kufuata ratiba ya shule. Hii ina maana kuwa ni muhimu kuthamini muda wa kuwahi katika shughuli za shule zilizopangwa katika ratiba na zilizopangwa na mwalimu wa zamu au kiongozi wa shule.

v) Mwanafunzi haruhusiwi kupiga kelele awapo darasani au eneo la shule.

vi) Mwanafunzi ni lazima kufanya mazoezi na mitihani yote itolewayo nje na ndani ya shule.

vii) Ni marufuku kwa mwanafunzi kutofika shuleni bila taarifa ya maandishi toka kwa mzazi/ mlezi.

**4. SARE YA SHULE**

i) Sare ya shule itavaliwa wakati wote mwanafunzi akiwa darasani, kazini, katika michezo na wakati wa safari kishule nje ya shule.

ii) Mwanafunzi anapaswa kuvaa sare ya shule iliyo safi, pia anapaswa kuwa msafi wa mwili.

iii) Wanafunzi hawaruhusiwi kutupa karatasi na uchafu wa aina yoyote ile katika shule.

iv) Kila mwanafunzi anapaswa kufanya usafi kikamilifu katika eneo la shule.

**5. MIPAKA YA SHULE**

i) Mwanafunzi haruhusiwi kuwa nje ya eneo la shule bila ruhusa maalumu.

ii) Ni marufuku kwa mwanafunzi kutembelea sehemu zifuatazo bila ruhusa.

a) Chumba cha Mwalimu

b) Ofisi za Shule

c) Nyumba za walimu

**6. NYONGEZA NAMBA 1 YA SHERIA ZA SHULE**

Ni marufuku kwa mwanafunzi kuwa na vitu vya thamani kwa matumizi binafsi kama:-

- Majiko na vifaa vingine vya kuchemshia maji au kupikia
- Simu ya aina yoyote ile.
- Radio na vifaa vinginevyo vya muziki.
- Kompyuta na viambata vyake.
- Runinga, Deki na Vinginevyo.
- Kamera za video na za kawaida.
- Radio za mfukoni, radio call n.k
- Dhahabu na vito.
- Vyakula
- Asije na nguo yoyote ya nyumbani. Atakayesemekana au kukamatwa na chochote kati ya hivyo atasimamishwa masomo.

**7. VIAMBATANISHO NA FOMU MUHIMU**

a) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination form) ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya Serikali.

Mwanafunzi apimwe Afya, **hasa mimba**, na kujaziwa kwenye fomu maalumu ya vipimo kabla ya kuja / Kuletwa shuleni.

b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi / Mkataba wa kutoshiriki katika Mgomo, Fujo na Makosa ya jinai.

c) Fomu ya mzazi kukiri kukabiliana na sheria, kanuni, kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

d) Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu na mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

## 8. Tafadhari soma kwa makini maelezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBUNI SANA ITILIMA SEKONDARI

Saini ya Mkuu wa Shule ______________________________

Jina la Mkuu wa Shule F. S. SHIMBI ______________________________

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI ITILIMA
S.L.P 194
BARIADI

Mhuri wa Mkuu wa Shule ______________________________

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

ANWANI YA MWANAFUNZI

…………………………………..

…………………………………..

MKUU WA SHULE,
SHULE YA SEKONDARI ITILIMA,
S.L.P 184,
**BARIADI**.

**YAH: <u>KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ITILIMA</u>**

Mimi ..................................................................................................... Ambaye ni mwanafunzi niliyechaguliwa kujiunga kidato cha …………………….. katika shule yako. Nakubali binafsi kujiunga na shule hii. Naahidi kuwa nitakuwa mwaminifu, mtiifu, nitafuata sheria za shule na nitazingatia taratibu zote za shule, nitatunza mali zote za Umma zilizopo hapo shuleni, nitasoma na kufanya kazi zote za shule kwa uwezo wangu wote na nitaishi kwa amani na kujiheshimu katika jumuiya ya shule na inayoizunguka shule.

………………………………
Sahihi ya Mwanafunzi

Mimi ………………………………………………………………………………………...…..…
Mzazi/ mlezi wa ...................................................................... mwanafunzi wa shule ya sekondari Itilima.

i) Mtoto wangu anafika shuleni na vifaa vyote alivyoagizwa na Shule.
ii) Kwa kipindi chote mtoto wangu atakapokuwa mwanafunzi wa Itilima nitashirikiana na Jumuiya ya shule kumsisitiza kufuata taratibu za shule.
iii) Mtoto wangu awapo nyumbani nitampatia muda na mazingira mazuri ya kujifunza na kufanya mazoezi aliyopatiwa na walimu wake (Home work) na nitamwelekeza pale ninapoweza.
iv) Nitawajulisha walimu mara moja mabadiliko yoyote mabaya katika tabia ya mtoto wangu, kwenda shule siku ambazo siyo za masomo bila Taarifa ya maandishi kutoka kwa uongozi wa shule nk.

……………………………………
**Sahihi ya Mzazi/ Mlezi**

**FORM NO. 1**

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

**PRESIDENT'S OFFICE**

REGIONAL ADMINISTRATIONS AND LOCAL GOVERNMENTS

**FORM FOR MEDICAL EXAMINATION**

To be completed by a medical officer in respect of all form I and form V entrants.

Student's full name
…………………………………………………………………………………...

Age/ Years ……………………………………………sex ………………………………………..

Blood found (red or white) ……………………………………………………………………...

Stool Examination ……………………………………………………………………………….

Urinalysis ………………………………………………………………………………………….

Venereal Disease test ……………………………………………………………………………

T.B test …………………………………………………………………………………………..

Ears ………………………………………………………………………………………...

Chest ………………………………………………………………….…………………

Spleen ………………………………………………………………………………………

Abdomen ……………………………………………………………………………………...

Urine for pregnant ……………………………………………………………………………….

ADDITIONAL INFORMATION (if any) e.g. Physical defects, impairment(s) e.g. arm, leg etc. infection chronic or family disease etc
…………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………

I certify that the above is fit to pursue further education as stated above.

Signature: …………………………………………………………………
Designation: ………………………………………………………………
Station: …………………………………… Date: ……………………..

Official Stamp: ………………………..……

**ANGALIZO: MWANAFUNZI AKIBAINIKA KUWA NA MIMBA AMBAYO MUDA WAKE UKAONESHA KUWA ALIIPATA KABLA YA KURIPOTI SHULE, NA FOMU YA VIPIMO IKAONESHA KUWA ALIJAZIWA KUTOKUA NA MIMBA, HATUA ZA KISHERIA ZITACHUKULIWA DHIDI YA DAKTARI ALIYEMJAZIA FOMU HIYO.**

## ORODHA YA VITABU

### 1. HISTORY

1. ADVANCED LEARNER'S HISTORY 5 & 6 - OXFORD
2. MASTERING HISTORY CARTER - CARTER
3. HISTORY FOR ADVANCED LEVEL - ZISTI KAMILI
4. CONTEMPORARY HISTORICAL EVENTS, HISTORY ONE-COMRADE SHIBITALI CK
5. CONTEMPORARY HISTORICAL EVENTS, HISTORY TWO-COMRADE SHIBITALI CK
6. HISTORY ONE REVISION BOOK-COMRADE SHIBITALI CK
7. HISTORY TWO REVISION BOOK- COMRADE SHIBITALI CK

### 2. GEOGRAPHY

1. PHYSICAL GEOGRAPHY - MSABILA
2. HUMAN ECONOMIC GEOGRAPHY - MSABILA
3. PHYSICAL GEOGRAPHY - MONK HOUSE
4. PHYSICAL GEOGRAPHY - BUNNET
5. INTERGRATED GEOGRAPHY - DAVID WAUGH

### 3. ENGLISH LANGUAGE

1. ADVANCED ENGLISH LANGUAGE - OXFORD
2. ENGLISH LANGUAGE - NICHOLAUS ASHEL
3. ADVANCED LITERATURE – NICHOLAUS ASHEL
4. OXFORD ADVANCED DICTIONARY
5. ENGLISH LITERATURE BOOKS
   - ✓ Encounters from Africa
   - ✓ Rwanda Magere
   - ✓ His Excellence The Head of States
   - ✓ I will marry when I want
   - ✓ Betrayal in city
   - ✓ Devine Province
   - ✓ A man of the people
   - ✓ The Beautyful Ones are not yet born
   - ✓ The wonderful surgeon
   - ✓ The Bride
   - ✓ Black Mamba
   - ✓ Selected poem

### 4. PHYSICS

1. PRINCIPLES OF PHYSICS FOR CLASS XI (S. CHAND'S)
2. PRINCIPLES OF PHYSICS FOR CLASS XII (S. CHAND'S)
3. ADVANCED LEVEL PHYSICS 7TH EDITION (MICHAEL NELKON)
4. ADVANCED PHYSICS (LOGER MANKASTER)

**5. BIOLOGY**

1. BIOLOGICAL SCIENCE FOR ADVANCED LEVEL 02nd or 03rd Edition
2. UNDERSTANDING BIOLOGY FOR ADVANCED LEVEL

**6. CHEMISTRY**

1. CONCEPTUAL CHEMISTRY - CHAND VOL. XI, XII
2. RAMSDEN - 04TH Edition

**7. ADVANCED MATHEMATICS**

1. PURE MATHEMATICS 1 & 2 - AUTHOR BACKHOUSE
2. ADVANCED LEVEL MATHEMATICS - C.J TRANTER
3. ADVANCED LEVEL MATHEMATICS - CHAND
4. ENGINEERING MATHEMATICS –
5. CONSCISE MATHEMATICS - BOSTOCK & CHANDLER

**8. KISWAHILI**

1. NADHARIA YA LUGHA KIDATO CHA TANO NA SITA-J.A MASEBO
2. KAMUSI YA KISWAHILI
3. NADHARIA YA LUGHA – C. M SALUHAYA
4. NADHARIA YA FASIHI –J.A MASEBO
5. RIWAYA;
    - ✓ KUFIKIRIKA-SHABAN ROBERT
    - ✓ USIKU UTAKAPOKWISHA-M. MSOKILE
    - ✓ VUTA n’KUVUTE-S.A .SHAFI
    - ✓ MFADHILI H. TUWA

**6. USHAIRI;**

- ✓ FUNGATE YA UHURU
- ✓ KIMBUNGA
- ✓ MAPENZI BORA
- ✓ CHUNGU TAMU

**7. TAMTHILIYA**

- ✓ NGUZO MAMA
- ✓ KWENYE UKINGO WA THIM
- ✓ MORANI
- ✓ KIVULI KINAISHI